BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA MBILI

Kikao cha Pili – Tarehe 29 Novemba, 2018.
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Waziri wa Fedha na Mipango

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Ukuzaji na Kulinda Vitega Uchumi Zanzibar Nam. 11 ya Mwaka 2004 na Kutunga Sheria ya Mamlaka ya Ukuzaji na Kulinda Vitega Uchumi Zanzibar na Kuweka Masharti Mengine Yanayohusiana na Hayo.

Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kuhusu Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Ukuzaji na Kulinda Vitega Uchumi Zanzibar Nam. 11 ya Mwaka 2004 na Kutunga Sheria ya Mamlaka ya Ukuzaji na Kulinda Vitega Uchumi Zanzibar na Kuweka Masharti Mengine Yanayohusiana na Hayo.

II. MASWALI:

Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:

95. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:

Pamoja na jitihada za Serikali katika kuleta maendeleo ya wananchi wa Zanzibar, lakini sekta ya mazingira bado lipo tatizo kubwa la kukabiliana na kujikinga na maafa yanayotokana na kubadilika kwa mifumo ya kuishi na tabia nchi.

(a) Je, Serikali imechukuwa hatua gani katika kukabiliana na maafa yanayotokezea katika bahari.

(b) Je, Serikali imechukuwa hatua gani katika kukabiliana na maafa yanayotokana na mafuriko katika njia za kupitisha maji.

(c) Je, Serikali imechukuwa hatua gani katika kukabiliana na janga la maradhi ya miripuko.

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

50. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Wananchi wengi wa Zanzibar wamefurahia uamuzi wa Serikali kugatua baadhi ya shughuli zake ikiwemo elimu, afya na kilimo kwa kuzipeleka kwa Serikali za mitaa. Hata hivyo, lipo tatizo kubwa la vyoo katika skuli nyingi za msingi na kati kwa kuwa na vyoo vibovu na vichache kulingana na wingi wa wanafunzi katika skuli hizo.

(a) Kwa kuwa hali hiyo inatishia afya za walimu na wanafunzi wao Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga vyoo katika skuli hizo.

(b) Wilaya ya Magaharibi “A” na “B” zinaongoza kwa kuwa na wanafunzi wengi kwenye skuli zake. Je,

Serikali ipo tayari kutoa kipaumbele katika ujenzi wa vyoo katika skuli za Wilaya hizo.

Wizara ya Fedha na Mipango:

37. MHESHIMIWA OMAR SEIF ABEID (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

Kwa kuwa SMZ ina hisa yake 20% kwa Kampuni ya Simu ya mkononi ya Zantel. Na kwa kuwa Kampuni hiyo inajiendesha kibiashara na kujipatia faida kwa kuuza huduma zake za simu sambamba na huduma za mawasiliano ya mkonge wa taifa.

(a) Je, Serikali imepokea kiasi gani cha gawio la faida "*dividend*" la huduma za simu na kiasi gani cha faida kutokana na mkonge wa taifa.

(b) Kwa mwaka 2017/2018, Kampuni ya simu ya Zantel imepata faida kiasi gani na Je, SMZ imepata kiasi gani kwa mujibu wa hisa inayomiliki.

(c) Je, ni upi ushirikishwaji wa SMZ kwenye uendeshaji wa kampuni hiyo ya Zantel ili Serikali iweze kutambua uhalisia wa biashara hiyo na faida inayopatikana ili hatimae kuweka uwiano wa kupata gawio la faida kama inavyostahiki.

89. MHESHIMIWA SHEHE HAMAD MATTAR (Jimbo la Mgogoni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

Kutokana na jitihada wanazochukua, naipongeza Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na ZIPA na Taasisi zilizotekeleza agizo la "One Stop Centre".

(a) Je, hadi kikao hiki cha Novemba, 2018 Taasisi za Wakala wa Usajili wa Mali na Biashara (BPRA) na Mhandisi wa Majengo zimeshaweka Maofisa wao katika Mamlaka ya ZIPA.

(b) Je, suala la kupatiwa mafunzo ya uwelewa wa kazi zao za Uwekezaji na "One Stop Centre" limeshatekelezwa.

(c) Je, kwa Taasisi ambazo hazikuwa na ulazima wa kuwepo maofisa wao hapo ZIPA, watashiriki vipi na kwa urahisi katika kuwahudumia wawekezaji wetu nchini.

Wizara ya Biashara, na Viwanda:

115. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Viwanda:

Wizara inafanya uteuzi wa maofisa wa vipimo, hata hivyo uteuzi huo haukufuata Sheria ya Vipimo namba 4 ya 1983. Sheria hiyo inataka kuwepo na chombo cha kuwateua maofisa hao. Hivyo inapelekea maofisa hao kutokufanyakazi kinyume na sheria.

Je, Wizara inasemaje kuhusu hili.

Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto:

18. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto:

Naipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa juhudi zake za kutetea haki za wanawake na watoto. Pamoja na juhudi hizo bado suala la unyanyasaji wa kijinsia limekuwa ni changamoto kubwa katika visiwa hivi.

(a) Je, unyanyasaji umepungua au umezidi kwa asilimia ngapi kwa mwaka 2017/2018 ukilinganisha na miaka iliyopita.

(b) Je, ni sababu gani za kitaalamu zilizogundulika kusababisha kuongezeka kwa tatizo hili.

(c) Je, Serikali pamoja na juhudi zake, ina mpango gani wa haraka kukomesha suala hili.

Wizara ya Elimu Na Mafunzo ya Amali:

49. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Katika kuimarisha huduma za elimu, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilipitisha Sera ya Elimu ya mwaka 2006 kwa ajili ya kupanga mambo mbali mbali ya kutekelezwa kupitia sera hiyo. Miongoni mwao ni kuwepo kwa elimu ya maandalizi kwa watoto wote waliofikia umri wa kuanza masomo.

(a) Je, ni skuli ngapi za maandalizi zilizopo hadi hivi sasa.

(b) Ni walimu wangapi wa maandalizi kwa kila Wilaya ambao wameajirwa kwa kazi hiyo.

Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati:

6. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati:

Kumekuwa na tatizo la kukatika umeme mara kwa mara nchini kwetu hali ambayo inasababisha huduma nyingi za kimaisha kusimama. Hata hivyo, Serikali imenunuwa majenereta ya akiba ili yatumike pindi ukizimwa umeme lakini majenereta hayo hayawashwi umeme unapozimwa.

Je, kwanini majenereta yale yaliyonunuliwa kwa gharama kubwa hayatumiki yanapohitajika hasa nyakati za kuzimwa umeme.

21. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji, na Nishati :

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inastahili pongezi kwa kusikia kilio cha wananchi wa Michamvi na kupanga kuwafikishia maji matamu kupitia bajeti ya mwaka huu. Wananchi hao wamejitayarisha kujitolea kusaidia kazi za kufikisha huduma hiyo, hivyo wengi wao wataacha kazi zao za bamvua la uvuvi, kilimo na utalii ili kushiriki kazi hiyo ya maendeleo.

Je, ni lini mpango huo utatekelezwa ili wananchi hao wajipange mapema kabla ya bamvua halijaanza.

Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

118. MHESHIMIWA SAID OMAR SAID (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

Itajulikana kwamba katika kipindi cha nyuma viongozi wa juu wa Serikali walikuwa wakitembelea mabonde yote ya kilimo hasa ya mpunga kwa Unguja na Pemba wakati wa utayarishaji na uvunaji, jambo ambalo lilikuwa likileta hamasa kwa wakulima na uwajibikaji kwa Wizara ya Kilimo. Siku za hivi karibuni utaratibu huo hufanyika kwa baadhi tu ya maeneo yaliyo katika mpango wa Serikali na kuwaacha wakulima wakihangaika kutafuta matrekta na pembejeo.

(a) Je, Serikali haoni umuhimu wa kurejesha utaratibu huo kwa madhumuni ya kukuza kilimo.

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wakulima wasiokuwa katika mpango huo kuweza kulima kwa tija na kitaalamu.

Wizara ya Afya:

72. MHESHIMIWA SIMAI MOHAMED SAID (Jimbo la Tunguu) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kumekuwa na malalamiko juu ya watu wanaopata ajali na wale ambao wamefanyiwa uhalifu huwa hawapati matibabu mpaka wawe na PF3.

(a) Je, ni utaratibu gani unaotumika katika hospitali ili kuhakikisha mgonjwa anapata huduma ya haraka ili kunusuru maisha yake.

(b) Je, ni idadi gani ya watu wamepoteza maisha kutokana na kukosa huduma ya kwanza hasa baada kupata majeraha kutokana na ajali au shambulio.

Wizara ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale:

70. MHESHIMIWA ALI SULEIMAN ALI (Jimbo la Kijitoupele - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale

Licha ya vyombo vya habari vya Serikali ZBC RADIO na ZBC TV kuendesha vipindi mbali mbali na kutupatia habari na matukio nchini.

Je, Serikali haioni kuna umuhimu wa uboreshaji wa kutoa taarifa kupitia vyombo hivyo.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

85. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

Katika malengo yake Shirika la Meli kwa mwaka wa fedha 2018/2019 limepanga kufanya safari 276 za ndani na safari 8 za nje ya nchi yaani Comoro na Mombasa kwa kutumia Meli zake mbili MV. Mapinduzi II na MV. Maendeleo.

Je, meli hizo mpaka hivi sasa zimeshafanya safari ngapi.

III. HOJA ZA SERIKALI:

Waziri wa Fedha na Mipango:

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Ukuzaji na Kulinda Vitega Uchumi Zanzibar Nam. 11 ya Mwaka 2004 na Kutunga Sheria ya Mamlaka ya Ukuzaji na Kulinda Vitega Uchumi Zanzibar na Kuweka Masharti Mengine Yanayohusiana na Hayo - Kusomwa kwa Mara ya Pili.

Zanzibar, **(Raya Issa Msellem)**
29 Novemba, 2018. **KATIBU WA BARAZA.**